Kwa sababu yo yote ya msingi inapokuwepo haja ya kumwachisha/kuacha kazi mfanyakazi kila upande utampa taarifa kwa utaratibu ufuatao:—

<i>Muda kazini (miaka)</i>	<i>Taarifa ya Kuachi-Malipo baada ya shwa kazi kwa au ya taarifa: muda:</i>
----------------------------	---

Miaka 1—3	mwezi mmoja (1)	Mshahara mwezi mmoja
Zaidi ya miaka 3—6	miezi mitatu (3)	Mshahara miezi mitatu
Zaidi ya miaka 6	Miezi minne (4)	Mshahara miezi minne

7.0 Upunguzaji wa Wafanyakazi:

7.1 Pande zote mbili zinakubaliana kujizatiti katika kulinda nafasi za kazi zilizopo na kufanya kila juhudi kuzuia uwezekano wa kupunguza wafanyakazi ambao wana nafasi zao tayari katika ajira.

7.2 Upunguzaji wa wafanyakazi utachukua nafasi tu baada ya uongozi wa Kiwanda kushauriana na viongozi wa Tawi la OTTU Wilaya na baada ya kufikiria njia mbalimbali na kukabiliana na hali hiyo ikiwa ni pamoja na kuwahamisha wafanyakazi kutoka Idara moja kwenda nyingine mpaka hapo hali itakapokuwa nzuri au kama lazima kwa kuwapunguza pole pole.

7.3 Ikiwa njia zote zitashindikana kwa kadri ya ujio wake utaratibu wa "FILO" utafuatwa katika kupunguza wafanyakazi pamoja na zoezi hilo masuala muhimu yafuatayo yatatakiwa yatazamwe kwanza:—

- Juhudi
- Uwezo wa kufanyakazi, uzoefu n.k.
- Muda kazini
- Umri
- Masuala ya kifamilia na
- Wale wote wanaopunguzwa kazi wawe wa kwanza kurejeshwa kazini hali hii inapokuwa nzuri.

8:0 Saa za Kazi:

8:1 Kiwanda kitakuwa na siku 5 za kazi kwa juma moja la kazi. Jumamosi, Jumapili na Sikukuu zote zinazotambulikana Kitaifa zitakuwa ni siku za mapumziko rasmi.

8:2 Saa zote za ziada zinazozidi masaa 45 ya muda wa kawaida wa kazi kwa jumla utachukuliwa kwa malipo ya ziada (overtime) kadhalika kwa kazi zitakazofanywa nyakati za siku za kawaida za kazi na siku za sikukuu zitalipwa kwa mujibu wa utaratibu ufuatao:—

- Kwa siku za kawaida za kazi malipo ya ziada yatakuwa mara moja na nusu ya mshahara wa kawaida wa saa moja ya kazi kwa kila saa inayozidi.
- Kazi itakayofanywa nyakati za siku za mapumziko na sikukuu mfanyakazi atalipwa mara mbili ya mshahara wa saa kwa kila saa moja ya kazi ya ziada.

9:0 Vima vya Mishahara katika kila Kikundi na Nyongeza:

9:1 Mishahara ya kila vikundi na nyongeza za mishahara zinaambatanishwa katika ambatanisho 'A' la mkataba huu. Viwango vya mshahara vitabadilika kutegemea tamko la Serikali katika kipindi cha mkataba huu.

10:0 *Kustaafu:*

10:1 Pande zote mbili zinakubaliana kwamba kila mfanyakazi atakuwa na umri wa kustaafu iwapo umri wake wa kustaafu utafika anaweza kuomba kustaafu mapema endapo afya yake kwa kuthibitishwa na daktari itaonekana haiwezeshi kuendelea na kazi yo yote.

10:2 Mfanyakazi hataendelea kufanya kazi baada ya umri wa miaka 55 Umri kati ya 50 na 55 mfanyakazi anaruhusiwa kustaafu kwa hiari.

10:3 Mfanyakazi anayestaafishwa atakuwa na haki kupata taarifa ya miezi miwili au mishahara ya miezi miwili badala ya taarifa.

11:1 Mfanyakazi anayeachishwa kazi kwa mujibu wa Ibara ya 6:0 au 7:0 ama anayestaafishwa kwa mujibu wa Ibara ya 10:0 atakuwa na haki ya kupata kiinua mgongo maalum (Gratuity) ili mradi tu utumishi wake usiwe chini ya miaka mitatu kazini kwa mpango ufuatao:—

Umri kazini kuanzia	Umri kazini kikomo	Kiasi katika pato au Mshahara
Miaka mitatu na	Bila kupungua miaka 6	Mshahara wa miezi miwili
Zaidi ya miaka sita	Bila kuzidi miaka 10	Mshahara wa miezi mitatu
Zaidi ya miaka kumi	Bila kuzidi miaka 20	Mshahara wa miezi minne
Zaidi ya miaka ishirini katika utumishi		Mshahara wa miezi mitano

12:0 *Posho ya safari za Kikazi:*

12:1 Afisa/Mfanyakazi ambaye anatakiwa kwa mujibu wa ajira yake au kwa kutumwa kazi maalum kusafiri kutoka katika Station yake ya kazi kwenda nje atalipwa posho ya safari katika utaratibu ufuatao, kwa kuzingatia GN 366 ya 1990 na GN 43 ya 1992:—

(a) Ikiwa mfanyakazi atakuwa katika haki ya usafiri kwa njia yo yote inayojulikana atalipwa Sh. 600/-.

(b) Mfanyakazi afikapo pale aendapo kikazi ili mradi tu kazi hiyo haitazidi miezi mitatu atahesabiwa yupo katika shughuli za muda mfupi hivyo atastahili kulipwa posho (night out allowance) katika viwango vifuatavyo:—

Jiji	Manispaa Miji ya Mikoa	Miji ya Wilaya	Wilaya Ndogo	Vijijini
3,000/-	2,000/-	1,000/-	1,000/-	500/-

12:2 Viwango hivi vya posho vitalipwa ndani ya eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tu.

12:3 Viwango hivi vinaweza kubadilika wakati wo wote wa mkataba huu kwa kufuata tamko la viwango vya Serikali.

13:0 *Likizo ya mwaka:*

13:1 Katika utumishi wa miezi 12 (kumi na miwili) mfanyakazi atakuwa na haki ya likizo yenye malipo ya siku 28. Malimbikizo ya likizo yatakubaliwa ikiwa mfanyakazi ataomba kwa maandishi na kukubaliwa na uongozi (au uongozi) au iwapo uongozi utamtaka abakie kazini kwa sababu ya shughuli nyingi za kikazi.

13:2 Likizo ya mwaka itakuwa ni ya malipo ya nauli kusaidia gharama za usafiri kutoka sehemu afanyayo kazi mpaka nyumbani kwao kwa mapumziko (yeye na familia) wasiozidi 4, kiasi hiki cha malipo kitatolewa kila mwaka.

14:0 *Mwendo wa Mashauri/Migogoro:*

14:1 Mashauri/migogoro yo yote ya kikazi yatakayotokea mahali pa Mwajiri na Wafanyakazi sheria ya Usalama Kazini Na. 62 ya 1964 au Sheria ya Mahakama ya Kazi Na. 41 ya mwaka 1967 zifuatwe kufuatana na ujio wa mashauri au migogoro inayoweza kuzuka.

14:2 Mgogoro wa kikazi, mfarakano kazini na au malalamiko ya kawaida ya wafanyakazi yatashughulikiwa kwanza na Tawi la OTTU mahali pa kazi. Ikiwa hakuna ufumbuzi uliofikwa katika ngazi hiyo basi Katibu wa Wilaya wa OTTU ataingilia kati na hatimaye kwa Katibu wa Mkoa fiadi kwa Katibu Mkuu.

14:3 Mgogoro wa kazi utapata ufumbuzi wa Kisheria aidha mbele ya msuluhishi na inapolazimika na mahakama ya kazi uamuzi ambao ni wa juu na wa mwisho.

15:0 *Tija/Ufanisi:*

15:1 Pande zote zinakubaliana kuweka mipango ya kazi iliyo mizuri na kutoa elimu kwa wafanyakazi wa ngazi zote kuhusu hali yetu ya Kiuchumi na jinsi wao walivyo na jukumu kubwa katika kuliweka Taifa letu hai na imara kiuchumi.

15:2 Pande zote zinakubaliana pia kwamba ni wafanyakazi wenye ari tu ndiyo wanaweza kuweka shahada timilifu katika kujenga uchumi au huduma nzuri hivyo licha ya elimu, Jumuiya kwa kushirikiana na uongozi wataweka motisha kwa wafanyakazi wa idara au sehemu zote.

15:3 Kiwanda/Shirika litalipia/kitalipia asilimia 50% ya gharama ya chakula cha mchana kwa kila mfanyakazi ili aweze kuwa na nguvu ya kuzalisha kwa wingi.

15:4 Kituo cha kutunzia watoto wadogo wakati wa kazi kitawekwa kwa gharama nafuu na mwajiri.

15:5 Wafanyakazi wa kike wanaonyonyesha watapewa muda wa saa moja kila siku ili wapate kunyonyesha watoto wakati wa kazi.

15:6 Utaratibu kuhusu mipango ya motisha itawekwa kwa makubaliano ya pande zote mbili kwa kufuatana na waraka wa Serikali Na. 1 wa 1981 wa sera ya Tija mapato na Bei.

16:0 *Matibabu:*

16:1 Wafanyakazi na Familia zao watapata matibabu bure. Mwajiri atatoa Hati ya Tiba (sick sheet) kwa mfanyakazi mgonjwa kuwezesha kwenda kutibiwa katika Hospitali inayotambulikana kwa matibabu. Habari muhimu zinazohusu mahudhurio ya hospitali, ugonjwa, matibabu na maamuzi ya Daktari ni vitu ambavyo vinategemea kuwamo katika "Sick Sheet" ya mgonjwa.

16:2 Hati hiyo ni mali ya mwajiri inapaswa kurudishwa kwa taarifa na kumbukumbu za kifisi.

17:0 *Gharama za Mazishi:*

Gharama za mazishi zitatolewa kwa mfanyakazi anayefariki akiwa bado katika utumishi, mwenyewe, mke au watoto).

17:2 Mwajiri atatoa sanduku na sanda na shada la maua kwa mfanyakazi na kiasi cha Sh. 20,000/- fedha taslimu gharama nyingine za mazishi. Endapo mfanyakazi ndiye aliyefariki watapata Sh. 20,000/-.

18:0 *Kodi ya Nyumba:*

18:1 Mfanyakazi atalipwa fedha taslimu kumwezesha kulipa pango la nyumba au sehemu ya pango hilo kwa kiasi kinacholingana na agizo la serikali katika GN. 366 ya 1990 na GN 43 ya 1992.

19:0 *Ada za Wanachama:*

19:1 Ada za wanachama wa OTTU zitakatwa kutokana na asilimia mbili (2%) ya kipato cha kila mfanyakazi mwanachama na kiasi kama hicho kama malipo ya huduma za OTTU (OTTU Service Fees) kwa kila mfanyakazi asiye mwanachama wa OTTU na kuwasilishwa kwenye Makao Makuu ya Muungano wa Jumuiya ya Wafanyakazi kwa kupitia akiba Na. 1 ya OTTU iliyopo Benki ya Taifa ya Biashara, Tawi la *Kichwele Dar es Salaam.*

20:0 *Nguo za Kazi:*

20:1 Wafanyakazi wote katika taaluma zinazostahili sare watapata pair mbili pia watastahili kupata nguo za kuhifadhi miili kikazi.

21.0 *Likizo ya Ugonjwa na Malipo:*

21:1 Wafanyakazi watapata likizo ya ugonjwa wa kawaida ya malipo endapo watapatwa na maradhi wakiwa bado katika utumishi wa *Kudumu* kwa kuzingatia Ibara hii pande zote zinakubaliana kwamba wafanyakazi watastahili likizo ya ugonjwa kwa utaratibu ufuatao:—

Umri Kazini	Muda wa Mshahara Kamili	Muda wa Nusu Mshahara
(a) Wafanyakazi wenye umri wa mwaka mmoja (1) kazini	Miezi mitatu (3)	Miezi mitatu
(b) Wafanyakazi wenye umri wa miaka zaidi ya mitatu (3) mpaka sita (6)	Miezi sita	Miezi sita
(c) Wafanyakazi wenye zaidi ya miezi sita (6)	Miezi sita	Miezi sita

22:0 Mwajiri atakuwa na hiari ya kuendelea kumwajiri au kumlipa kiwango cho chote cha mshahara iwapo muda ulioonyeshwa hapo juu utakuwa umekwisha.

22:1 Mfanyakazi atakayeachishwa kazi kwa mujibu wa Ibara hii atalipwa kiinua mgongo kama kilivyochezwa katika Ibara ya 11:1 ya mkataba huu na haki nyingine zo zote anazostahili mfanyakazi anayeachishwa kazi kwa njia ya amani.

22:2 Likizo ya ugonjwa itatokana na mapendekezo ya Mganga anayetambuliwa na au kulazwa wodini kwa sababu ya ugonjwa isipokuwa ugonjwa unaotokana na uzazi kwa wafanyakazi wa kike.

22:3 Likizo ya Uzazi na likizo ya ugonjwa wa uzazi itatolewa kwa kuzingatia sheria na 1 ya mwaka 1975.

23:0 *Sahihi:*

23:1 Mkataba huu umewekwa sahihi leo tarehe 1 Januari, 1992.

Kwa ajili na kwa niaba ya

Muungano wa Jumuiya za Wafanyakazi Tanzania OTTU.

Sgd

Katibu wa OTTU Mkoa

Kwa ajili na kwa niaba ya Mwajiri

MALIKI'S AUTO GARAGE

Sgd.

Sgd.

Katibu wa OTTU Wilaya

Sgd

Mwakilishi wa Wafanyakazi

Tarehe 1 Januari, 1992

Sgd.

Shahidi wa Mwajiri

2/10/1992

Coram: Mackanja, J.

Assessors: J. V. Mwambuma — OTTU

Jully Kaonga — ATE

Menejiment: Amani Syc Kyejo — Storekeeper

Stumai Ismail — Katibu OTTU Tawi

C.C. — David, N.

TUZO

Mkataba umesajiliwa ukiwa na marekebisha katika aya 10.2, 12.1, 18.1. Unaanza kutumika tarehe Mosi Januari, 1992 kwa kuwa wahuusika hawakutaja tarehe ya kuanza kutumika katika aya ya 4.1. Mwajiri alete mahakamani mara moja kiambatisho "A" kilichotajwa katika aya ya 9.1.

Sgd.

J. M. MACKANJA,

2 October, 1992

Certified true copy of the original.

B. E. NYAMUBI,

Registrar

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 628

MAHAKAMA YA KAZI

MKATABA WA HIARI NA. VA. 1/91

baina ya

JUMUIYA YA WAFANYAKAZI TANZANIA (JUWATA)

na

REGIONAL TRADING CO. SINGIDA

Kwa kufuatana na sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3 Mkataba wa Hiari baina ya Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania Regional Trading Co, Singida uliotolewa mbele ya Mahakama ya Kazi (Permanent Labour Tribunal) na

Kutokana na mamlaka iliyotolewa kwa Mahakama ya Kazi kwa mujibu wa Sheria Na. 41 kifungu cha 7 fasili ya (b) na makubaliano ya pamoja na washauri wa Mahakama (Assessors) Mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa ukiwa na makubaliano yaliyokubaliwa na pande zote mbili.

1. *Utangulizi:*

1.1 Sisi Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania (JUWATA) tujulikanao kama Umoja wa Wafanyakazi na RTC Singida tujulikanao hapa kama mwajiri kwa hiari zetu na katika hali ya maclewano tumefikia makubaliano katika masuala mbalimbali yaliyomo katika kumbukumbu hii ambayo yanaweka hali bora zaidi za kazi zikiwamo nyongeza za mishahara katika kila ngazi na vikundi vya wafanyakazi walioajiriwa na Kampuni.

2.0 Utambuzi:

- 2.1 (a) Jumuiya ya wafanyakazi wa Tanzania inawatambua RTC Singida kwamba ndio waajiri pekee ambao wameajiri wafanyakazi ambao pia ni wanachama wake.
- (b) Kadhalika RTC Singida wanaitambua Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania kuwa ndio chombo pekee cha wafanyakazi kinachotetea maslahi yao.
- 2.2 Kwa ujumla kila chombo kimoja kinatambua kuwepo kwa chombo kingine kisheria na kwamba wafanyakazi huwa ni kiungo kikubwa cha ushirikiano baina yao.
- 3.0 **Wahusika:**
- 3.1 Mkataba huu utawahusu wafanyakazi wote wa kudumu wa Kampuni isipokuwa wale waliopo katika uongozi. Viongozi kwa mujibu wa Mkataba huu huu ni kama ifuatavyo:—
- (a) Meneja/Meneja Mkuu (Mwenye Mkataba Maalum)
- (b) Mameneja wa Miradi au Wakuu wa Idara (wenye Mkataba Maalum).
- (c) Wataalamu wa taaluma mbali mbali (Wenye Mkataba Maalum).
- 4.0 **Muda wa Tarehe ya Kuanza kwa Mkataba:**
- 4.1 Pande zote mbili zimekubaliana kwamba Mkataba huu uanze kuheshimiwa kuanzia tarehe mosi mwezi Julai mwaka wa elfu moja mia tisa tisini na kudumu kwa muda wa miezi 12 (kumi na mbili). Upande wowote utakaokusudia kufuta kifungu chochote au kuongeza au kufanya marekebisho yoyote katika Mkataba huu unaweza kufanya hivyo kwa kuupa taarifa ya miezi mitatu upande wa pili na kuendelea sababu za makusudi hayo.
- 4.2 Mkataba unaweza kubadilishwa wakati wowote ndani ya kipindi cha miezi 12 ili mradi tu upande wowote wenye kusudio la kufanya hivyo uwe umearifu upande mwingine makusudi ya kufanya hivyo.
- 4.3 Mkataba huu utaendelea kuheshimiwa hata baada ya muda uliowekwa katika para 4.1 ya Ibara hii iwapo hapatakuwa na upande utakaowahi kutoa taarifa kwa upande mwingine kwa makusudi ya kutengeneza upya Mkataba huu.
- 5.0 **Ajira:**
- 5.1 Wafanyakazi wa kudumu wa Kampuni wataajiriwa kwa mshahara wa mwezi katika masharti ya kudumu baada ya kupitia utaratibu ufuatao:—
- (a) **Majaribio:**
- (i) Wafanyakazi wote watakuwa katika majaribio ya miezi kumi na mbili kabla ya kuajiriwa katika masharti ya kudumu katika ajira/taaluma wanayohusika.
- (ii) Mfanyakazi atakayepandishwa cheo chenye madaraka atakuwa katika majaribio ya miezi sita.
- (b) **Kuthibitishwa:**
- (i) Baada ya kumaliza vyema muda wa majaribio mfanyakazi atapata barua ya kuthibitishwa katika ajira yake.
- (ii) Asipomaliza vema muda wa majaribio utaongezwa kwa miezi sita. Iwapo baada ya muda huo utendaji wake wa kazi bado hauridhishi basi ataachishwa kazi.
- 5.2 Ajira ya Wafanyakazi wa muda itaendelea kuwapo tu kwa kazi ambazo hazidumu kwa zaidi ya miezi mitatu.
- 6.0 **Kuacha au Kuachishwa kazi:**
- 6.1 Kwa sababu yoyote ya msingi, inapokuwepo haja ya kumuachisha kazi mfanyakazi, taarifa ya kuwaachisha kazi itatolewa kulingana na sheria za kazi za Nchi.

- 6.2 Mfanyakazi anayetaka kuacha kazi baada ya kuthibitishwa kazini atatoa taarifa kama ilivyofafanuliwa katika para 6:1 ya Ibara hii.

7.0 Upunguzaji wa Wafanyakazi:

- 7.1 Pande zote mbili zinakubaliana kujidhatiti kulinda nafasi za kazi zilizopo na kufanya kila juhudi kuzuia uwezekano wa kupunguza wafanyakazi ambao tayari wana nafasi zao tayari katika ajira.
- 7.2 Upunguzaji wafanyakazi utachukua nafasi tu baada ya uongozi wa Kampuni kushauriana na viongozi wa Tawi, na JUWATA Wilaya na baada ya kufikiria njia mbalimbali za kukabiliana na hali hiyo ikiwa ni pamoja na kuwahamisha wafanyakazi kutoka Idara moja kwenda nyingine mpaka hapo hali itakapokuwa nzuri au kama lazima kuwapunguza pole pole.
- 7.3 Ikiwa njia zote zitashindikana kwa kadri ya ujio wake utaratibu wa "FILO" utafuatwa katika kupunguza wafanyakazi. Pamoja na zoezi hilo masuala muhimu yafuatayo yatatakiwa yatazamwe kwanza.
- (a) Juhudi.
- (b) Uwezo wa kufanyakazi, uzoefu n.k.
- (c) Muda kazini.
- (d) Umri
- (e) Masuala ya kifamilia na
- (f) Wale wote wanaopunguzwa kazi wenye ufanisi mzuri wawe wa kwanza kurejeshwa kazini hali inapokuwa nzuri.
- 8.0 **Saa za Kazi:**
- 8.1 Kampuni itakuwa na siku sita za kazi kwa juma moja la kazi lenye jumla ya masaa ya kazi 40 tu. Jumapili na Sikukuu zote zinazotambuliwa kitaifa zitakuwa ni siku za mapumziko rasmi.
- 8.2 Saa zote za ziada zinazozidi masaa 40 (zilizo dhinishwa na mwajiri) ya muda wa kawaida wa kazi kwa juma utachukuliwa kwa malipo ya ziada (overtime) kadhalika kwa kazi zitakazofanywa nyakazi za sikukuu. Kazi itakayofanywa nyakati za sikukuu, zitalipwa kwa mujibu wa utaratibu ufuatao:—
- (a) Kwa siku za kawaida malipo ya ziada yatakuwa mara moja na nusu ya mshahara wa kawaida wa saa moja ya kazi kwa kila saa inayozidi.
- (b) Kazi itakayofanywa nyakati za siku za mapumziko na sikukuu mfanyakazi atalipwa mara mbili ya mshahara wa saa kwa kila saa moja ya kazi ya ziada, kufuatana na Sheria ya marupurupu Na. 152 ya mwaka 1972 pamoja na marekebisho yake.
- 9.0 **Vima vya Mishahara katika kila Kikundi na Nyongeza:**
- 9.1 Mishahara ya kila vikundi inaambatanishwa katika Ambatisho "A" la Mkataba huu.
- 9.2 Pande zote mbili zimekubaliana ya kwamba nyongeza ya mshahara ya mwaka 1990/91 itakuwa kulingana na nyaraka za SCOPO zilizopo.
- 10.0 **Kustaafu:**
- Pande zote mbili zinakubaliana kwamba kama mfanyakazi atakuwa na umri wa kustaafu iwapo umri wake wa kustaafu utafikiwa au, anaweza kuomba kustaafu mapema endapo afya yake kwa kuthibitishwa na daktari itaonekana haimwezeshi kuendelea na kazi yoyote.
- 10.1 Mfanyakazi hataendelea kufanya kazi baada ya umri wa miaka 55. Umri kati ya 50—55 kwa mfanyakazi anaruhusiwa kustaafu kwa hiari.

10.2 Mfanyakazi anayestaafishwa kazi katika umri wa kati ya miaka 50—55 atakuwa na haki ya kupata taarifa ya miezi sita au mishahara ya miezi minne badala ya taarifa.

10.3 Mfanyakazi anayestaafu kazi atapewa zawadi kulingana na uwezo wa Kampuni.

11.0 *Kiinua Mgongo (Gratuity):*

Mfanyakazi anayeachishwa kazi kwa mujibu wa Ibara ya 7.0 ama anayestaafishwa kwa mujibu wa Ibara ya 10.0 au mfanyakazi akifariki dunia mrithi wake atakuwa na haki ya kupata kiinua mgongo maalum (gratuity) ili mradi tu utumishi wake usiwe chini ya miaka mitatu kazipi kwa mpango ufuatao:—

Umri Kazini Kuanzia	Umri kazini Kikomo	Kiasi katika pato au Mshahara
Zaidi ya miaka mitatu	bila kupungua miaka 6	Mshahara wa miezi 2
Zaidi ya miaka sita	bila kupungua miaka 10	Mshahara wa miezi 3½
Zaidi ya miaka 20 katika utumishi		Mshahara wa miezi 8½

12.0 *Posho ya Safari za Kikazi:*

12.1 Afisa/mfanyakazi ambaye anatakiwa kwa mujibu wa ajira yake au kwa kutumwa kazi maalum kusafiri kutoka katika station yake ya kazi kwenda nje atalipwa posho ya safari katika utaratibu ufuatao:—

Mahali	PSS 1-6 PRS 7-10 PGS 11-13	PRS 1-3 PGS 8-10	PRS 1-3 PGS 4-7	PGS 1-3 POS 1-9	Safarini
Jiji na Manispaa	4,000/-	3,500/-	3,000/-	2,500/-	1,500/-
Miji Mikuu ya Mikoa	3,700/-	3,200/-	2,700/-	2,200/-	1,500/-
Miji Mikuu ya Wilaya	3,400/-	2,900/-	2,400/-	1,900/-	1,500/-
Miji Midogo	3,100/-	2,600/-	2,100/-	1,600/-	
Vijijini	1,000/-	1,000/-	1,000/-	1,000/-	

Watoto wapate asilimia hamsini (50%) ya kiwango cha mzazi kwa kundi linalohusika.

13.0 *Likizo ya Mwaka:*

13.1 Kila mfanyakazi atachukua au kupewa likizo yake ya mwaka kufuatana na masharti kama ilivyoelezwa katika maagizo ya SCOPO Na. 2 na 19 isipokuwa idadi ya watoto wa kulipiwa nauli isizidi watoto wanne © (4). Na sheria ya marupuru G.N. 336 ya mwaka 1990 pamoja na marekebisho yake.

13.2 *Likizo ya Ugonjwa na Matibabu:*

13.3 (a) Matibabu yatatolewa bure na Kampuni kwa wafanyakazi, mke na watoto wanaomtegemea.

(b) Wafanyakazi watakaolazimika kupata matibabu kwenye Hospitali nje ya Kampuni watapelekewa barua ya kitambulisho ikihitajika.

(c) ikiwa mfanyakazi itabidi alazwe hospitali basi kanuni za SCOPO juu ya daraja zitafuatwa.

(d) Iwapo mfanyakazi atahitajika kupimwa, atalazimika kuonyesha taarifa ya uchunguzi wa Mganga Mkuu wa Serikali wakati wowote anapotakiwa kufanya hivyo.

13.4 *Likizo ya Uzazi:*

13.5 Likizo ya uzazi itatolewa kama ilivyo katika agizo Na. 20 la SCOPO na badiliko la sheria ya Bunge Na. 1 1975 fungu la 25.B.

13.6 *Likizo ya Ugonjwa na Malipo:*

13.7 Wafanyakazi watapata likizo ya ugonjwa kwa kawaida ya malipo endapo watapatwa na maradhi wakiwa bado katika utumishi wa Kampuni. Kwa uzingatifu wa Ibara hii pande zote zinakubaliana kwamba wafanyakazi wataastahili likizo kwa viwango kulingana na kanuni za SCOPO kwa watumishi wa mashirika ya Umma.

13.8 Mwajiri atakuwa na hiari ya kuendelea kumwajiri au kumlipa kiwango chochote cha mishahara iwapo muda ulioonyeshwa katika mpango huo hapo juu utakuwa umekwisha.

13.9 Mfanyakazi atakayachishwa kazi kwa mujibu wa Ibara hii atalipwa kiinua mgongo kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 11.1 ya mkataba huu na haki nyingine zozote anazotahili mfanyakazi anayeachishwa kazi kwa njia ya amani.

13.10 Likizo ya ugonjwa itatokana na mapendekezo ya mganga anayetambulikana na au, kulazwa wodini kwa sababu ya ugonjwa unaotokana na uizazi kwa mfanyakazi wa kike.

13.11 *Likizo ya Dharura:*

13.12 Iwapo mfanyakazi atafiwa na jamaa yake, akiwa baba mzazi, Mke/Mme au mtoto, atapewa likizo ya dharura ya malipo ya siku saba ambayo haitakatwa katika likizo yake ya mwaka.

14.1 *Mwenendo wa Mashauri/Migogoro:*

Mashauri/Migogoro yoyote ya kikazi yatakatwa mahali pa kazi kati ya mwajiri na wafanyakazi, sheria ya Usalama Kazini Na. 62 ya 1964 na au, sheria ya Mahakama ya Kazi Na. 41 ya mwaka 1964 zinaweza kufuatwa na ujio wa mashauri au migogoro inayoweza kuzuka.

14.2 Mgogoro wa kikazi, mfarakano kazini na au malalamiko ya kawaida ya wafanyakazi yatashughulikiwa kwanza na tawi la JUWATA mahali pa kazi. Ikiwa hakuna ufumbuzi uliofikiwa katika ngazi hiyo basi Katibu wa Wilaya ataingilia kati, kutoka kwa Katibu wa Wilaya Mkoa hadi kwa Katibu Mkuu iwapo hakuna ufumbuzi wa amani unaofikiwa katika ngazi zote hizo ndipo Katibu Mkuu atakapotakiwa kutaarifu mgogoro wa Kikazi.

14.3 Mgogoro wa kazi utapata ufumbuzi wa kisheria aidha mbele ya msuluhishi na Mahakama ya Kazi uamuzi ambao ni wa juu na wa mwisho.

15.0 *Tija/Ufanisi:*

15.1 Pande zote zinakubaliana kuweka mipango ya kazi iliyo mizuri na kutoa elimu kwa wafanyakazi wa ngazi zote kuhusu hali yetu ya kiuchumi na jinsi wao walivyo na jukumu kubwa katika kuliweka taifa letu hai na imara kiuchumi.

15.2 Pande zote zinakubaliana pia kwamba ni wafanyakazi wenye ari tu ndio wanaoweza shabaha timilifu kujenga uchumi au kutoa huduma nzuri, hivyo licha ya elimu Jumuiya kwa kushirikiana na uongozi utajiweka motisha kwa wafanyakazi wa Idara au cha sehemu zote.

16.0 *Gharama za Mazishi:*

16.1 Gharama za mazishi zitatolewa kwa mfanyakazi anayefariki akiwa bado katika utumishi na au jamaa ya mfanyakazi, akiwa mke, mme, mama mzazi, baba mzazi, au mtoto.

16.2 Mwajiri atatoa sanduku na sanda au Shs. 10,000/- (chochote kilicho chini) kwa yeyote wa jamaa ya mfanyakazi kama ilivyo fafanuliwa katika ibara Na. 16.1 na kiasi cha Sh. 6,000/- fedha taslimu kwa gharama

nyinginezo za mazishi. Endapo mfanyakazi ndiye aliyefariki, jamaa ya mfanyakazi watapata mahitaji yote ya mazishi na fedha taslimu Sh. 15,000/-. Mwijiri atatoa usafiri wa maiti ya mfanyakazi, mke au mtoto wa umri kati ya miaka 5 hadi 16 kupelekwa kijijini kwake.

17.0 Nyuma za Wafanyakazi:

17.1 Imekubaliwa kwamba Kampuni ya Biashara ya Mkoa itafuata sera ya Taifa ya Tija, Mapato na Bei kwa Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi kama kifungu 50 (b) cha sera hiyo kinavyoagiza.

18.0 Ada za Wanachama:

Ada za wanachama wa JUWATA zitakatwa kutokana na asilimia moja (1%) ya kipato cha kila mfanyakazi mwanachama na kiasi hicho kama malipo ya huduma za JUWATA (Service fees) kwa kila mfanyakazi asiye mwanachama wa JUWATA na kuwasilishwa kwenye Makao Makuu ya Jumuiya ya Wafanyakazi kwa kupitia Akiba Na. 1 ya JUWATA iliyopo Benki ya Taifa ya Biashara, Tawi la Market Street, S.L.P. 9944, Dar es Salaam.

19.0 Nguo za Kazi:

19.1 Wafanyakazi waliomo katika taaluma zifuatazo wanastahili kupata sare au nguo za kuhifadhi miili kikazi. WALINZI, WASAIDIZI WA MADEREVA, MAFUNDI, MABOHARIA WATUNZAJI SARUJI.

20.0 Vishawishi:

20.1 Pande zote mbili tumekubaliana kwamba kutakuwa na mpango wa kuwachagua wafanyakazi HODARI NA BORA kila mwaka ambao watapewa vyeti vya JUWATA vya Mfanyakazi HODARI NA BORA. Pia mwajiri atampa mfanyakazi huyo kiasi cha Sh. 500/- au zaidi kama tunzo.

20.2 Mwijiri ataweka (Board of Honour) ambapo picha za wafanyakazi HODARI NA BORA wa kila mwaka zitatundikwa kwa kumbukumbu na heshima yao.

21.0 Elimu kwa Wafanyakazi:

21.1 Pande zote mbili zimekubaliana ya kwamba Kampuni ya Biashara ya Mkoa itaendelea:—

- i) Kufuta kutokujua kusoma na kuandika kwa wafanyakazi wote wa Kampuni ya Biashara ya Mkoa.
- (ii) Kuongeza ujuzi wa kazi za kitaalamu au kuwaendeleza wafanyakazi katika mbinu za utendaji bora wa kazi zao.
- (iii) Kuwaendeleza wafanyakazi ki-michezo, ki-starehe na ki-utamaduni.

21.2 Iwapo mfanyakazi atashinda mtihani au daraja la kazi yake basi itabidi kumpa nafasi ya juu ili mradi tu haya yafuatayo yatazingatiwa:—

- (i) Nafasi;
- (ii) Sifa;
- (iii) Juhudi na muda wa kazi.

23.0 Sahihi:

23.1 Mkataba huu umetiwa sahihi leo tarehe

Kwa ajili na kwa niaba ya
JUMUIYA YA WAFAN-
NYAKAZI TANZANIA

Kwa ajili na kwa niaba ya
KAMPUNI YA BIASHARA
YA SINGIDA

(Sgd. Lahmoud Masoud)
Katibu wa Mkoa

(Sgd. F. G. Lyiku)
Meneja Mkuu

(Sgd. H. M. Nyachia)
Katibu wa Juwata (Wilaya)

(Sgd. A. S. Kyando)
Meneja Masoko

(Sgd.)

Katibu wa Juwata (RTC)

(Sgd. A. F. Londo)

Meneja Maendeleo ya Utumishi
Uendeshaji

25/3/1992

Coram: J. M. Mackanja, Jaji.

TUZO

Mkataba huu unasajiliwa ukiwa na marekebisho yaliyofanyika, na unakuwa na nguvu kukidhi utashi wa waliousani kwa niaba ya waliowawakilisha.

(Sgd. J. M. Mackanja, Jaji)
Mwenyekiti

Certified true copy of the original.

(B. E. Nyamubi)
Msajili

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 629

MGOGORO WA KIKAZI NA. 19 WA 1992.

MUUNGANO WA VYAMA VYA WAFANYAKAZI
TANZANIA (OTTU) VS MAMLAKA YA BANDARI

UAMUZI

Mackanja, J.

Mamlaka ya Bandari Tanzania, kwa nyakati mbali mbali, iliwasimamisha kazi au kuwafukuza kazi watumishi kadhaa kwa kutumia vizuri au vibaya mamlaka yake chini ya Sheria ya Usalama Kazini, 1964. Sasa hivi si mhimu kuamua iwapo mamlaka hayo yalitumia vizuri au hapana. Sasa hivi ni kuona kama Mahakama ya Kazi ina mamlaka na uwezo wa kusikiliza shauri hii. Haupo upande wowote uliotoa hoja kuhusu suala hili; lakini nimeona nililifumbie macho kwa kuwa ni suala la sheria.

Kifungu cha 28 cha Sheria ya Usalama Kazini kinasema:—

“(1) No suit or other civil proceeding (other than to enforce a decision of the Minister or the Board on a reference under this Part shall be entertained in any civil court with regard to the summary dismissal or proposed summary dismissal....of an employee”.

Ukiondoa baraza la usuluhishi na Waziri wa Kazi, Mahakama zenye mamlaka ya kusikiliza mashauri ya madai zimenyimwa uwezo wa kusikiliza mashauri yatokanayo na kufukuzwa kwa wafanyakazi chini ya Sheria ya Usalama Kazini. Hali hii ya sheria ilisisitizwa na Mahakama ya Rufaa katika *Mwanza Textiles Ltd. vs. Augustine Masatu (CA) Civil App. Na. 8 of 1988*. Mamlaka pekee ambayo yamebakia kwenye mahakama hizo ni kusikiliza mashauri yatokanayo na utekelezaji wa maamuzi ya baraza la usuluhishi au Waziri wa Kazi. Mamlaka hayo yamo katika kifungu cha 27 cha Sheria ya Usalama Kazini. Kifungu hiki kinazipa mahakama zenye mamlaka ya kusikiliza mashauri ya madai uwezo wa kutekeleza maamuzi ya baraza la usuluhishi au Waziri wa Kazi kana kwamba maamuzi hayo ni hukumu za mahakama hizo. Mamlaka hayo ni pamoja na kutekeleza amri zinazomtaka mwajiri kufidia mishahara, na kadhalika.

Mamlaka ya mahakama zenye uwezo wa kusikiliza kesi za madai katika kukaza hukumu yamo katika Order XXI ya The Civil Procedure Code. Mahakama ya Kazi imepewa uwezo wa kutekeleza maamuzi yake kwa kufuata utaratibu huu. Ingawa mamlaka hayo yametolewa, sheria haiendelei mbele kusema kwamba Mahakama ya Kazi inayo mamlaka ya kuteleza maamuzi ya chombo kingine chochote.

Kutokana na hali hii ya sheria, nina mashaka makubwa kama kwa hakika mahakama hii inayo mamlaka ya kusikiliza malalamiko ambayo yametokana na kupishana kwa tafsiri ya sheria kati ya mwajiri na walalamikaji katika kutekeleza maamuzi yaliyotolewa chini ya Sheria ya Usalama Kazini. Naona mamlaka hayo hatuna. Kutokana na umuhimu wa hoja zilizotolewa, Mahakama hii itatoa, declaratory decision tu kama mwongozo wa wadaawa. Baada ya kusema hayo sasa natoa uamuzi ambao utazingatia hoja zote ambazo zinabishaniwa.

Mgogoro wa kikazi ulio mbele ya Mamlaka unatokana na Mamlaka ya Bandari Tanzania (T.H.A.) na azma ya mwajiri kukataa kuwalipa wafanyakazi nusu mshahara walionyimwa wakati wamesimamishwa kazi ama kwa kuwa walikuwa wanakabiliwa na mashtaka ya nidhamu au mashtaka ya jinai, baada ya wafanyakazi Tanzania kushindwa kukubaliana na mwajiri juu ya suala hili, uongozi wa JUWATA ulilitaka Baraza Kuu la Majadiliano, ambalo limeundwa kujadili masuala ya uhusiano kati ya mwajiri na wafanyakazi kupitia JUWATA, ili Baraza hilo litoc ufafanuzi. Katika Kikao cha 27 cha Baraza hilo kilichofanyika Tanga tarehe 12 na 22 Machi, 1989 (Kiambatisho Na. 2 katika hati ya madai), baada ya kuzisikia hoja za JUWATA na za mwajiri, chombo hicho kiliigiza menejimenti walifanyie utafiti suala hili baada ya kubainika kwamba zipo hukumu mbili za Mahakama Kuu ambazo zinatoa kauli tofauti juu ya stahili ya malipo ya nusu mshahara pale ambapo mfanyakazi aliyekuwa amesimamishwa kazi kwa nusu mshahara anaporejeshwa kazini.

Baraza Kuu la Majadiliano lilifanya kikao chake cha 28 tarehe 30 Novemba hadi tarehe 2 Desemba 1989 huko Mtwara ambapo kikao hicho kililirejea suala hili. Katika kikao hicho, kulingana na Kiambatisho Na. 3 cha hati ya madai, liliagiza kwamba:—

“3.20.1 Kama ilivyoelezwa na Menejimenti katika kikao kilichopita kwamba endapo kuna hukumu mbili za mahakama zilizopitishwa na majaji wenye hadhi sawa mwajiri anaweza kufuata hukumu ile yenye Appeal Na. 8 ya 1986 iliyotolewa na Jaji H. (sic) Mnzavas inapingana na hukumu iliyotolewa Jaji Patel J. (sic) (1978) LRT 28 Mamlaka haina msingi wa kutekeleza dai la JUWATA la kuwalipa malimbikizo ya nusu mshahara wale walioshinda kesi.

“3.20.2. Mwenyekiti alidokeza kwamba suala hili linahusu wafanyakazi ...katika mashirika mengi, kikwazo pia kwa suala hili kipo SCOPO ambaye (sic) inaelekeza kutolipwa malimbikizo, ya nusu mshahara kwa wafanyakazi aliyeshinda kesi ya jinai.

3.20.3. Baada ya ufafanuzi wa Tanzania Legal Corporation kusomwa, Baraza lfmekubaliana kwamba JUWATA katika ngazi ya Taifa walifanyie kazi suata hili ili kupata msimamo.

Na katika kikao chake cha 29 kulingana na Kiambatisho Na. 4 cha hati ya madai Baraza Kuu la Majadiliano lilielekeza kwamba:

“ii....JUWATA waendele kutafuta ufumbuzi wa kisheria kuhusu suala la kutolipwa nusu mshahara”.

Huo ndio ulikuwa mwisho wa majadiliano, na sasa JUWATA inatafuta ufumbuzi wa mfarakano baina yao na mwajiri hapa mahakamani. Katika kikao chake cha 32 kilichofanyika tarehe 14 hadi 15 Desemba, 1990 hapa Dar es Salaam, JUWATA ilitoa taarifa juu ya azma yao ya kulileta shauri lao hapa; Baraza lilipokea taarifa hiyo na likakubaliana na JUWATA kuhusu hatua walizokusudia kuchukua dhidi ya mwajiri katika kufanikisha madai yao.

Hayo ndiyo madai ya JUWATA. Baada ya kuyatafakari, Nd. P. Moshā Mshauri kutoka Muungano wa Jumuiya za Wafanyakazi Tanzania (OTTU) na Nd. K. Komba, Mshauri kutoka Chama cha Waajiri Tanzania, walimshauri kwamba hoja zinazojitokeza na masuala yanayobishaniwa yanaweza kushughulikiwa kwa ufasaha zaidi kwa njia ya hoja za maandishi. Mimi niliyakubali maoni hayo; kwa ajili hiyo niliwaagiza wawakilishi wa wadaawa waletē hoja za maandishi.

Katika hoja zao za mdai, JUWATA (sasa OTTU) wanadai kwamba mwajiri hana haki ya kumkata mfanyakazi malipo ya mshahara wake katika kipindi ambacho hakufanya kazi ILA kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Kazini. Isitishie, mwajiri kwa hiari yake mwenyewe alimzuia kila mfanyakazi mhusika asifanye kazi. Aidha, OTTU wanadai kwamba pale ambapo mfanyakazi anarejeshwa kazini na Baraza la Usuluhishi au na Waziri anayesimamia masuala ya kazi, au pale ambapo anaonekana hana hatia ya kosa la jinai lililokuwa likimkabili mahakamani, kusimamishwa kazi kwa mfanyakazi kunabatilishwa. Kwa hiyo anakuwa na haki ya kulipwa nusu mshahara kipindi chote alipokuwa amesimamishwa kazi. OTTU wametaja mashauri kadhaa yaliyoamuliwa na Mahakama ya Rufaa Tanzania pamoja na Mahakama Kuu Tanzania ambayo wanaamini yanaiunga mkono hoja yao. Mashauri hayo yatachambuliwa baadaye wakati wa kutafakari hoja za mwajiri kwa kuwa hukumu katika mashauri haya haya zimetumiwa na mwajiri kuimarisha hoja zake.

Baada ya kutoa historia ya mgogoro huu, hususan uamuzi wa Baraza Kuu la Majadiliano, na baada ya menejimenti kuona kwamba suala hili ni la kisheria na siyo la majadala na mapatano jinsi JUWATA walivyoona, mwajiri anatoa hoja kwamba kukataa kwake kulipa nusu mshahara hakutokani na ufedhuli isipokuwa kinatokana na misingi ya sheria. Katika hoja zake mwajiri anadai kwamba haki za wafanyakazi wote siyo sawa mbele ya sheria, kutegemea ajira zao na mkondo wa sheria wanaofuata katika matatizo yao ya kikazi. Kwa mfao wapo wanaorejeshwa kazini:—

- (i) kwa amri ya Waziri wa Kazi (au baraza la usuluhishi);
- (ii) kwa kushinda kesi zao mahakamani; na
- (iii) Kwa hiari ya mwajiri baada ya kufanya uchunguzi katika tuhuma zilizosababisha mfanyakazi huyo asimamishwe kazi.

Katika hoja zake mwajiri anatafautisha jinsi ya kumshughulikia mfanyakazi aliyerejeshwa kazini kwa amri ya Waziri (au baraza la usuluhishi) na yule aliyerejeshwa kazi ni kwa hiari au ridhaa ya mwajiri, kwa upande mmoja; na kwa upande mwingine, ni mfanyakazi aliyeshinda kesi mahakamani. Kwa maoni yake, wafanyakazi wanaoangukia katika kundi la kwanza (ambao wanajumuisha waliorejeshwa kazini kwa amri ya Waziri au baraza la Usuluhishi, na wale waliorejeshwa kazini kwa ridhaa ya mwajiri) wana haki ya kuhesabiwa mshahara au ujira kwa kipindi waliposimamishwa kazi. Wanaoangukia katika kundi hili wanaporejeshwa kazini mwajiri anadai kwamba hawastahili kupewa malipo yoyote ya ujira kwa mantiki kwamba mwajiri anayo haki ya kisheria kukata malipo ya mshahara kwa kipindi ambacho mfanyakazi hakufanya kazi. Kwa madai yake mwajiri anaona kwamba kundi linalosalia, yaani wanaorudishwa kazini baada ya kushinda kesi zao mahakamani, hawana haki yoyote kisheria wala kimkataba kulipwa malipo mengine ya nusu mshahara. Tutaona baadaye kwamba msimamo huu unatokana na tafsiri ya Katibu na Sheria ya Usalama Kazini ambayo mwajiri anadhani zinamuunga mkono.

Aidha, mwajiri anaegemea Kanuni F. ya Kanuni za Utumishi katika Mashirika ya Umma (Parastatal Service Regulations), zamwaka 1984. Kanuni hii, kabla ya kusahihishwa, ilitamka kwamba mfanyakazi anaporejeshwa

kazini baada ya kushindwa kesi mahakamani bastahili kulipwa nusu mshahara ambayo mwajiri alikuwa anazuia wakati wa kipindi cha mashtaka hayo. Kamati ya Rais ya Kusimamia Mashirika ya Umma (SCOPO) iliyotoa kanuni hizi ilitoa sahihisho kulingana na Waraka wake Kumb. Na. KMU/S.11/G.24 wa tarehe 10 Agosti, 1992 ambao umetolewa kama kiambatisho "C" cha hati ya utetezi. Katika Waraka huo SCOPO inakiri kwamba Agizo lake la kuzuia nusu ya mshahara-

"... linapingana na Sheria ya Usalama Kazini ya mwaka 1964 iliyorekebisha na sheria Na. 1 ya mwaka 1975 Kifungu 29(3)..... inayomtaka mwajiri kumlipa mfanyakazi mtuhumiwa nusu mshahara wake pamoja na marupurupu mengine kwa kipindi chote alichokuwa amesimamishwa kazi ikiwa itabainika kwamba hana hatia na kuamiriwa arejeshwe kazini....."

Mwajiri anadai kwamba marekebisho yaliyofanywa na SCOPO ni batili kwa kuwa yanapingana na Katiba ya nchi na hayalingani na sheria ya Usalama Kazini, hasa chini ya kifungu cha 29(3) na kifungu cha 40A(4). Pale ambapo maagizo ya SCOPO yanapingana na sheria za nchi, maagizo hayo hubatilika na badala yake sheria ndiyo hufuatwa.

Hoja ya mwisho ya mwajiri inatokana na dhana yake juu ya mkataba wa ajira, kwamba mfanyakazi atastahili malipo chini ya mktaba huo pale ambapo amefanya kazi. Hakuna malipo bila kazi, isipokuwa kama pale mwajiri anapomruhusu mfanyakazi kwenda likizoni, anapokuwa mgonjwa. Kwa madaai yake hoja hii inatokana na mantiki kwamba likizo ni mapumziko kwa ajili ya ufanisi wa kazi na ugonjwa kuhesabiwa kama sehemu ya silika ya binadamu isiyozuilika. Vinginevyo mfanyakazi hastahili malipo bila kuyafanyia kazi kwanza.

Baada ya kutafakari masuala yanayobishaniwa Mahakama inakubaliana na mwajiri kwamba masuala yafuatayo ndiyo hoja kuu ambazo uamuzi wake ndio utakaokuwa umetataua masuala yote ambayo umetolewa na wadaawa, yaani:-

1. Iwapo mfanyakazi aliyesimamishwa kazi na mwajiri anayo haki ya malipo kamili kwa kipindi chote alichosimamishwa kazi, baada ya kurudishwa kazini kwa agizo la Waziri wa Kazi au Baraza la Usuluhishi;
2. Mfanyakazi aliyesimamishwa kazi kwa tuhuma za makosa ya nidhamu, na hatimaye akarejeshwa kazini kwa ridhaa ya mwajiri anastahili kulipwa mshahara kamili baada ya kurejeshwa kazini.
3. Ni nini stahili ya mfanyakazi aliyesimamishwa kazi wakati anakabiliwa na mashtaka ya jinai, na hatimaye akarejeshwa kazini baada ya kushinda kesi katika kesi hiyo ya jinai? Je, anayo haki ya kulipwa nusu mshahara iliyokuwa inazuiwa na mwajiri wakati mfanyakazi huyo alipokuwa amesimamishwa kazi kwa nusu mshahara?
4. Je Mkataba wa ajira katika Shirika la Umma unaruhusu malipo bila kufanya kazi? Kama jibu ni ndiyo, halali kisheria?

OTTU wameleta hoja fupi lakini fusaha kuhusu masuala yanayobishaniwa, ikiwa ni pamoja na kunukuu hukumu katika kesi moja. Hoja za kina zimetolewa na wakilishi wa mwajiri. Mahakama inawapongeza wawakilishi wa wadaawa maana mchanganuo waliotoa juu ya masuala yanayobishaniwa umegusa mambo muhimu ambayo yamkuwepo kwa muda mrefu. Baadhi ya masuala hayo yamefanywa uamuzi, na mengine bado. Kwa hiyo tunatarajia kwamba uamuzi wa hoja hizi utaweka pamoja mambo mengi ya kisheria.

Tutaanza na hoja ya mwanzo, yaani iwapo mfanyakazi aliyesimamishwa kazi na mwajiri anayo haki ya kulipwa mshahara kamili kwa kipindi chote alichosimamishwa kazi baada ya kurudishwa kazini kwa amri ya Waziri au kwa amri ya baraza la usuluhishi.

Wakili wa mwajiri anadai kwamba sheria inayotoa ufumbuzi wa hoja hii ni Katiba ya Muungano wa Jamhuri ya Tanzania, hasa Ibara Na. 11, 15, 22, 23, 25, 26 pamoja na vifungu vya 25, 26 na 40A vya Sheria ya Usalama Kazini.

Ibara ya 11 ya Katiba inatamka kwamba Mamlaka ya Nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kufanya kazi, utaratibu ambao utahakikisha kwamba kila mtu anaishi kwa jasho lake. Ibara ya 15 inazungumzia uhuru wa mtu na kuishi kwa uhuru; Ibara hii inapiga marufuku mtu kukamatwa na kuziliwa bila kosa. Hata bila kuitolea maelezo zaidi Ibara hii iko wazi; haina uhusiano na haki ya mtu kufanya kazi pamoja na wajibu wake wa kula jasho lake. Ibara za 22, 23, 25 na 26, kwa pamoja zinatoa fursa na haki sawa kwa watu wote kushika nafasi yoyote ya kazi; haki ya kupata ujira unaolingana na kazi aifanyayo na kwamba watu wote wanaofanya kazi watapata malipo kulingana na kiasi na sifa za kazi waifanyayo; kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii Katiba; na kwamba haitakuwapo kazi ya shuruti.

Haupo ubishi; nami nakubaliana na Wakili wa mwajiri, kwamba Katiba ndiyo Sheria Kuu ya Nchi; kila mtu analazimika kuitii na kutekeleza yale yanayoagizwa na Katiba hiyo. Ni sahihi pia kwamba sheria yoyote inayokiuka Katiba ni batili; lakini kwa kufuata Katiba hiyo sioni ni wapi panapompa mwajiri haki ya kuwafukuza kazi wafanyakazi wasio na makosa na wanaporejeshwa kazini na mamlaka halali mwajiri atafute kinga ya kuwapa haki ambayo walistahili kama mwajiri asingekuwa ametumia vibaya mamlaka yake. Ipo tofauti kubwa kati ya mfanyakazi ambaye amecha kazi mwenyewe halafu baadaye akakubaliwa kurejeshwa kazini, na yule aliyefukuzwa kazi halafu mamlaka halali yakaamua arejeshwe kazini. Katika mfano wa kwanza mfanyakazi huyo hatakuwa na haki ya kulipwa ujira katika muda alipojiondoa kazini. Katika mfano wa pili mfanyakazi aliyecondolewa kazini kwa amri ya mwajiri ana kosa gani linalohalalisha anyimwe stahili yake? Maana yeye alikuwa tayari kufanya kazi lakini mwajiri akamshurutisha asiifanye kazi. Sheria zetu ziko wazi kwa wale wanaoshurutishwa wasifanye kazi, wakati wao wako tayari kutimiza wajibu wao chini ya mkataba wa ajira. Kifungu cha 16 cha Sheria ya Uajiri; Sura 366 kiko wazi juu ya suala hili. Sehemu muhimu za kifungu hicho inasema:-

"...every employer shall, unless the employee has broken his contract of service...., provide his employee with work in accordance with the contract during the period for which the contract is binding...., and if the employer fails to provide work as aforesaid he shall pay to the employee.... wages at the same rate as the employee had performed a day's work."

Mantiki nyuma ya sheria hizi ni kwamba pale ambapo mfanyakazi ana mkataba wa ajira, atakuwa na haki ya kuendelea kufanya kazi hiyo mpaka pale mwajiri atakapovunja mkataba huo kwa njia halali na mamlaka yaliyopewa uwezo wa kuamua shauri litakalotokana na hatua ya mwajiri yatakapoithibitisha hatua itakayokuwa imechukuliwa na mwajiri. Kwa mtazamo huo vifungu vya Katiba alivyonukuu Wakili wa mwajiri hakukusudia kuwabana wafanyakazi walioonewa na mwajiri, wao; vimekusudiwa kuwadhibiti wazururaji ambao hawako tayari kujilisha kutokana na jasho lao. Kwa misingi hiyo ningeamua kwamba Katiba ya Muungano wa Jamhuri ya Tanzania haiathiri haki za wafanyakazi wanaoshinda kesi za jinai au mashauri ya nidhamu dhidi yao. Maana kifungu cha 29(3) cha Sheria ya Usalama Kazini kinachoweka utaratibu wa malipo nusu mshahara wakati mfanyakazi amesimamishwa kazi hakikiuki Katiba; kifungu hiki kinakidhi utashi wa Ibara ya 11 na ya 23 ya Katiba ambazo zinaiagiza Mamlaka ya Nchi kuweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha

utetekelezaji wa haki ya mtu kufanya kazi pamoja na haki ya kupata ujira unaolingana na kazi yake na kwamba kila mtu anayefanya kazi, ikiwa ni pamoja na aliye na mkataba wa ajira ambao umesimamishwa kwa kitendo cha mwajiri kisicho halali, anastahili kupata malipo ya haki.

Mwajiri anatoa hoja pia, kwamba mfanyakazi anayerejeshwa kazini na baraza la usuluhishi au na Waziri wa Kazi hana haki ya kulipwa nusu ya mshahara uliokuwa unazuiwa na mwajiri kutokana na kauli ya kifungu cha 25(1)(a), 26(2) na 40(A)(4) vya Sheria ya Usalama Kazini. Mwajiri anatoa hoja, kwa usahihi kabisa kwamba mfanyakazi anayerejeshwa kazini anapewa haki ya malipo ya mshahara na haki nyingine zinazoambatana na malipo hayo. Kwa urahisi wa kumbukumbu sheria hiyo nitanukuu, nayo inasema, sehemu ambazo ni muhimu, kwamba:—

“S.25”—(1) Where, in the exercise of its powers under this Part, a Board orders—

- (a) the re-engagement or re-instatement of an employee.... the employer shall re-engage or re-instate the employee in his former employment, and such re-engagement or re-instatement shall have effect for the purpose of payment of wages.... from the date of the employee's summary dismissal or suspension.... but the employer may deduct from any wages due on or after any re-instatement any half pay paid during the period of suspension.”

Kwa lugha ya Kiswahili kifungu hiki kinasema kwamba pale ambapo baraza la usuluhishi linapamuru kwamba mfanyakazi aajiriwe upya (re-engagement) au arejeshwe kazini (re-instatement), mwajiri analazimika kumwajiri upya au kumrejeshwa kazini mtumishi huyo katika nafasi aliyokuwa nayo kabla ya kufukuzwa kazi au kusimamishwa kazi, kwamba mfanyakazi atalipwa mshahara tangu siku alipokufukuzwa kazi au aliposimamishwa kazi; bali mwajiri anaweza kukata sehemu yoyote ya mshahara aliyokuwa anamlipa tangu mfanyakazi afukuzwe kazi au tangu asimamishwa kazi kutoka katika limbikizo la mishahara au ujira huo. Tafsiri ya sheria hii ni hizi: mwajiri anaamriwa kumrejeshwa mfanyakazi kazini; hatua ya pili ni kwa mwajiri kutekeleza amri hiyo (labda kama anakata rufaa); mfanyakazi atakaporipoti kazini mwajiri analazimika kumlipa mfanyakazi huyo Mishahara na marupurupu yote ambayo angekuwa analipwa kama angekuwa kazini. Wakati wa kumlipa mfanyakazi huyo mwajiri anaweza kukata nusu ya mshahara ambao alikuwa anamlipa mfanyakazi wakati amesimamishwa kazi. Hii ina maana kwamba, kama mshahara wa mfanyakazi ni Sh. 2,000/- kwa mwezi, mfanyakazi huyo anaposimamishwa kazi kwa nusu mshahara atalipwa Sh. 1,000/-. Wakati anaporejeshwa kazini mwajiri analazimika kumlipa Sh. 2,000/- kwa kila mwezi alikuwa amesimamishwa kazi, bali atakuwa na hiari ya kumkata Sh. 1,000/- alizokuwa akimlipa kama nusu mshahara. Kwa hiyo mfanyakazi atakuwa na haki ya kupokea mshahara baada ya kuondoa nusu ya mshahara alikuwa akilipwa.

Utaratibu huu umewekwa kwa madhumuni ya adhabu zinazotolewa chini ya Kigawe cha III cha Sheria ya Usalama Kazini. Utaratibu mwingine umewekwa na kifungu cha 40A ambacho kimo katika Kigawe cha IV. Utaratibu uliowekwa na Kigawe cha III ndio utekelezaji wake unaambatana na Kanuni ya Nidhamu. Utaratibu uliowekwa na kifungu cha 40A unaziba pengo ambalo lilikuwapo wakati ambapo wafanyakazi wanafukuzwa kazi bila kujaziwa Fomu Na. 1 hadi Na. 10. Yametolewa matukio sita ambamo utaratibu huu utatumika. Aya ya (4)(a) ya kifungu cha 40A kinalipa baraza la usuluhishi, na Waziri wa Kazi baada ya kusikiliza rufaa,

uwezo wa kumwamuru mwajiri amrejeshwa, au amwajiri upya mfanyakazi sawa na kifungu cha 25(1)(a) kinavyosema, isipokuwa kifungu hiki cha 40A(4)(a) kinaongeza kusema kwamba:—

“...but the employer may deduct from any wages due on or after the re-instatement, the wages in respect of the number of days during which the employee remained absent from work (and including) the day on which the termination or dismissal took effect and the day on which the re-instatement is ordered....”

Sheria hii inampa mwajiri, mbali na kumkata mfanyakazi nusu mshahara aliyolipwa wakati alipokuwa amesimamishwa kazi, uwezo wa kumkata mfanyakazi; mshahara kwa siku zote ambazo hakuwa kazini ikiwa ni pamoja na siku ambapo alifukuzwa au alipoachishwa kazi na siku ambapo amri ya kumrejeshwa kazi inatolewa.

Tafsiri ya kifungu hiki iko hivi: Mwajiri anamfukuza kazi mfanyakazi; baraza la usuluhishi au Waziri wa Kazi anaamuru kwamba mfanyakazi huyo arejeshwe kazini. Mwajiri atamrejeshwa kazini na atamlipa limbikizo la mishahara pamoja na marupurupu mengine ya kazi sawa na hali ilivyo katika utaratibu uliowekwa na kifungu cha 25(1)(a). Licha ya kumkata nusu ya mshahara alikuwa akimlipa, mwajiri pia anaweza kumkata mshahara mfanyakazi huyo kwa siku zote ambazo alitakiwa kuwa kazini lakini akawa hakufika. Siku hizo zimetajwa kujumuisha siku ambapo hakuna kazini kabla, na pamoja na, siku alipofukuzwa kazi au alipoachishwa kazi; siku nyingine ambapo hatalipwa mshahara ni ile anapotakiwa kurejea kazini na asifike kazini kuendelea na kazi. Mfanyakazi awezi kukataa mshahara kwa siku ambazo hakuwa kazini akitumikia adhabu itakayobatilishwa na baraza la usuluhishi kwa kuwa hakutakiwa kuwa kazini. Kwa hiyo ni siku ambazo hakuwa kazini kabla ya kufukuzwa kazi na siku anayotakiwa kurejeshwa kazini ndizo. pekee mwajiri ana haki kumkata mfanyakazi mshahara na siyo muda wote kati ya kufukuzwa kazi na anaporejeshwa kazini. Tafsiri na hii haitaleti mantiki iliyokusudiwa kumlinda mfanyakazi anayeadhibiwa bila makosa. Mfano ni hivi: mfanyakazi anakaa nje ya kazi siku tatu na anafukuzwa kazi siku ya nne; siku hizo halipwe mshahara. Baadaye baraza la usuluhishi linamrejeshwa kazini na linamwagiza aendelee na kazi siku maalum inawekwa; Hatalipwa mshahara siku hiyo kama hataripotiti kazini. Siku nyingine zote kati ya siku anapofukuzwa na siku anaporejeshwa kazini stahili yake na kulipwa mshahara haiathiriki.

Tafsiri ya kifungu cha 25(1)(a) na kifungu cha 40A(4) vya Sheria ya usalama Kazini imezingatia kusudio la mkataba wa kazi, ambao una masharti sawa na mikataba mingine. Madhumuni ya mkataba ni kuweka bayana haki na wajibu walioingia mkataba huo: Kwa hiyo pale ambapo upande mmoja unavunja mkataba ili kukwepa wajibu wake, au kwa visingizio, sheria inalinda haki za mshiriki wa mkataba huo ambaye hana makosa. Hiyo ndiyo mantiki katika hukumu ya keşi ya *Measures Brothers, Ltd. vs Measures* (1970) 2Ch. 248 ambao mahakama ilisema:—

“...it is elementary justice that one of the parties to a contract shall not get rid of his responsibilities thereunder by diabling the other contractor from fulfilling his part of the bargain.”

Hukumu hii ingetatsiriwa kwamba ni haki ya kimsingi kuwa mshiriki mmoja katika mkataba hatakwepa wajibu wake chini ya mkataba huo kwa kumzuia mshiriki mwenzake asitekeleze wajibu wake katika mkataba huo. Kwa hiyo si haki kwa mwajiri kama mshiriki katika mkataba wa ajira kukwepa wajibu wake kwa kuuvunja mkataba huo. Ingawa hukumu hii ilitolewa Uingereza, ninaafikiana nayo kutokana na hekima iliyomo humo. Kwa kuzingatia hekima hiyo Mahakama Kuu

ya Tanzania ilitoa kauli ifuatayo; ilipokuwa inatoa hukumu katika kesi ambamo mlalamikiwa alikuwa ndiye mrufani, katika *Tanzania Harbours Authority vs Wendelin Ludger (DSM) HC Civil Appeal No. 8 of 1986*:

"...The appellant wrongly suspended the respondent from work and now turns round and says that the respondent is not entitled to his salary because he did not work for him. Surely, and rightly argued by the learned defence counsel, once an employee is found not guilty and acquitted in a criminal case which was the basis of his suspension from work, he is automatically re-instated "in his work....."

Once there is re-instatement the employee is, under section 25(1) of Cap. 574, entitled to all his rights as the contract of employment has revived with all its incidents".

Hukumu katika rufaa hii ilitolewa na Mnzavas, J. K., alivyokuwa wakati huo.

Katika misingi ya hukumu hii pia mwajiri havezi kukwepa kumlipa mfanyakazi limbikizo la nusu mshahara ambao atakuwa anamkata wakati mfanyakazi mhusika amesimamishwa kazi.

Mbele ya Mahakama hiyo hiyo ipo hukumu nyingine ambayo inatoa kauli kwamba mfanyakazi hastahili nusu ya mshahara aliyokuwa anakatwa wakati amesimamishwa kazi katika kipindi cha mashtaka ya jinai, Kesi hiyo iliyohukumiwa na Patel, J., ni *Yusuf Mzowa vs A. Spagnaletti*, (1978) LRT n. 28. Nakubaliana na Mnzavas J. K. alivyokuwa, kwamba hukumu hiyo imepitwa na wakati kwa kuwa haikuzingatia hali halisi ya sheria: *Labour Laws, (Miscellaneous Amendments) Act, No. 1 of 1975* ambayo imerekebisha kifungu cha 40A(4) cha Sheria ya Usalama Kazini ambacho tayari tumeona jinsi kinavyolinda haki za washiriki katika mkataba wa ajira.

Japokuwa tumeona kuwa wafanyakazi waliosimamishwa kazi kwa nusu mshahara wana haki ya kurejeshwa kazini kwa mshahara kamili, haki hiyo itakamilika iwapo tu chombo kinachoamuru kurejeshwa kwao kazini kinaamuru pia kwamba alipwe limbikizo la mshahara. Hii ndiyo kauli ya Mahakama ya Rufaa Tanzania katika shauri la *Mwanza Textiles Ltd. vs Agostine Masatu*, (CA) Civil Appeal No. 8 of 1988 ambamo katika ukurasa wa 3 wa hukumu inasema:—

"The order of the Minister directed the re-instatement of the respondent in his former employment. It did no more no less. Any remedy therefore for payment of arrears of salary lay elsewhere...."

Kama baraza la usuluhishi au Waziri wa Kazi hatatamka katika uamuzi wake kwamba mfanyakazi anarejeshwa kazini kwa malipo kamili katika muda mfanyakazi huyo alipokuwa amesimamishwa kazi, au alipokuwa nje baada ya kuachishwa au kufukuzwa kazi, malipo ya mshahara wakati wa kipindi hicho hayana budi kudaiwa kwa taratibu zilizowekwa chini ya Kigawe cha XI cha Sheria ya Uajiri, Sura 366.

Kwa upande mwingine, na kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi katika Mashirika ya Umma, 1984 Kanuni F.3 ambayo ilikuwa inatumika wakati malalamiko haya yanaletwa mahakamani hapa inatamka wazi kwamba mfanyakazi aliyesima nishwa kazi atapokea nusu ya mshahara wake mpaka hapo uamuzi wa mwisho utakapotolewa. Kama mashtaka ya nidhamu au mashtaka ya jinai yameanzishwa dhidi ya mtumishi huyo na akaonekana hana makosa, Agizo la SCOPO Kumb. Na. KMUS/11/9/64 la tarehe 10 Agosti 1992 ambalo linarekebisha Kanuni F.3 linamwagiza kila mwajiri katika mashirika ya umma kulipa nusu mshahara uliobakia baada ya mfanyakazi kuonekana hana hatia na kurudishwa kazini.

Huo ndio msimamo wa sheria. Kwa upande wa Washauri wametoa maoni ambayo yanaoana na hali halisi ya sheria ilivyo. Nd. K. K. Komba, Mshauri kutoka Chama cha Waajiri Tanzania, ametoa maoni kwamba haoni mgongano wowote kati ya Katiba na sheria kuhusiana na haki ya mfanyakazi kulipwa nusu mshahara aliyokuwa akikatwa, baada ya kesi ama ya jinai au ya nidhamu itakayokuwa inamkabili. Ameendelea kusema kwamba haki za mfanyakazi aliyesimamishwa kazi husimama kwa muda wakati yeye mwenyewe amesimamishwa kazi, mpaka hatima ya mashtaka dhidi yake itakapojulikana. Kwa mantiki hiyo kama mfanyakazi atashinda kesi yake na ikaamriwa arejeshwe kazini, basi inampasa mwajiri kumlipa mfanyakazi huyo nusu ya mshahara ambayo alikuwa anakatwa wakati amesimamishwa kazi kwa kuwa ajira yake itakuwa imerudia hali yake ya awali. Kwa hali hiyo wafanyakazi katika mgogoro huu wana haki ya kulipwa nusu mshahara uliobaki; kauli hii haitawahusu wale walioacha kazi wenyewe kabla ya uamuzi juu ya tuhuma dhidi yao kufikiwa. Hivyo mwajiri hakuwa na msingi wowote wa kisheria wa kukataa kuwalipa wadau nusu mshahara.

Mrs. P. Masha, Mshauri kutoka Muungano wa Jumuiya za Wafanyakazi Tanzania, kimsingi hana mtazamo tofauti. Sawa na nilivyosema katika mchanganuo wa hoja zinazobishaniwa, naye anaona kwamba suala kubwa linaloleta mvutano katika mgogoro huu ni la kutafsiri sheria. Mshauri huyo anaona kwamba vifungu vya Katiba vilivyotajwa na mwakilishi wa mwajiri havifai kunukuliwa kwa mazingira ya kesi za wafanyakazi katika mgogoro huu. Kwa maoni yake, Mshauri huyu anasisitiza umuhimu uliopo kwa mwajiri kutofautisha kati ya mfanyakazi aliyeshindwa kufanya kazi kwa kusababishwa na mwajiri, yaani mwajiri anapomzuia asifanye kazi kwa kumsimamisha kazi. Katika mgogoro huu wafanyakazi hawakuamua wao wenyewe kutofanya kazi, walisimamishwa kazi na mwajiri kutokana na tuhuma za makosa mbali mbali. Ameongeza kusema kwamba, kwa manuno mengine, wafanyakazi walinyimwa haki ya kufanya kazi kutokana na sababu zisizokuwa na uhakika. Kwa hiyo uamuzi wa baraza la usuluhishi, au ule wa Waziri wa Kazi, wa kuwarudisha kazini pamoja na mahakama kuwaachia huru wafanyakazi hao unafanya wasipoteze haki yoyote kuhusiana na ajira yao. Aidha, kulingana na waraka wa SCOPO wa tarehe 10 Agosti, 1992 mashirika ya umma hayana budi kuwalipa nusu mshahara unaokatwa wakati wafanyakazi wamesimamishwa kazi iwapo watarejeshwa kazini.

Kutokana na maoni haya Washauri wanashauri nitamke kwamba mwajiri awalipe walalamikaji stahili zao za nusu mshahara na marupurupu mengine waliyonyimwa wakati wamesimamishwa kazi kabla ya kurejeshwa kazini. Kutokana na ushauri huu, pamoja na mchanganuo wa hoja na tafsiri ya sheria, ninayaafiki maoni hayo. Kutokana na mwafaka huo nazijibu hoja zilizokuwa zikibishaniwa kama ifuatavyo:—

1. Hoja ya 1 na 3 zinafanana. Zitajibiwa pamoja. Mfanyakazi anayerejeshwa kazini kwa amri ya baraza la usuluhishi au kwa amri ya Waziri wa Kazi ana haki ya kulipwa nusu mshahara pamoja na marupurupu mengine aliyokuwa ananyimwa wakati amesimamishwa kazi. Stahili hii itategemea uamuzi wa baraza la usuluhishi au Waziri wa Kazi unazema nini. Kama uamuzi huo hautamwagiza mwajiri amrejeshe kazini mfanyakazi pamoja na haki anazostahili chini ya sheria itakuwa hiari ya mwajiri kulipa haki hizo baada ya kumrejesha kazini mfanyakazi mhusika. Pale ambapo baraza la usuluhishi au Waziri wa Kazi hawakumwagiza mwajiri alipe haki hizo na mwajiri akakataa kuzilipa, mfanyakazi mhusika atalazimika kutafuta njia nyingine ya kudai haki hizo, ikiwa ni pamoja na kufuata utaratibu uliowekwa na Kigawe cha XI cha Sheria ya Uajiri, sura 366.

2. Pale ambapo mwajiri kwa uamuzi wake atamsimamisha kazi mfanyakazi, na baadaye amrejeshe kazini bila kumwadhibu, haki za mfanyakazi hazitaathirika kwa kuwa ni mwajiri atakuwa amemzuia mfanyakazi kutekeleza wajibu wake chini ya mkataba wa ajira. Kwa kutimiza masharti ya mikataba, anayevunja mkataba ndiye analazimika kulipa fidia; hivyo mwajiri atalazimika kumuweka mfanyakazi katika hali ambamo angekuwa kama mwajiri asingekuwa ameusimamisha mkataba wa ajira. Mfanyakazi anakuwa katika hali ambamo angekuwa tu kwa kulipwa stahili ambazo angepata kama asingezuiliwa kufanya kazi kwa kitendo kisichohalali cha mwajiri. Kama mwajiri atakataa kuzilipa haki hizo, mfanyakazi anaweza kuzidai chini ya taratibu zilizowekwa na sheria za kazi.

3. Kulingana na Kanuni za Utumishi katika Mashirika ya Umma ambazo zilikuwa zikitumika wakati mgogoro huu ulipoanza, waajiri wote wanaotawaliwa na Kanuni hizo, akiwemo mlalamikiwa katika shauri hili, wanalazimika kuwalipa wafanyakazi nusu mshahara waliokuwa wamezuia wakati mfanyakazi amesimamishwa kazi. Kanuni hizi zina nguvu za kiuendeshaji tu; hazina nguvu sawa na sheria, ingawa kuzikiuka kwa ukaidi au kwa ufedhuli kunaweza kusabisha makosa ya nidhamu.

Kutokana na sababu nilizotoa pamoja na ushauri niliopewa na Washauri, Mahakama ya kazi ina tamka kwamba walalamikaji wanastahili kulipwa haki wanazodai kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa katika uamuzi huu. Uamuzi huu wa tamko unaweka wazi hali halisi ya sheria ila hautekelezwi kwa kuwa Mahakama ya Kazi haina mamlaka chini ya Sheria ya Usalama Kazini.

Uamuzi huu umetolewa hapa Dar es Salaam, leo Alhamisi tarehe 8 Aprili, 1993.

(Sgd. J. M. MACKANJA, JAJI).
Mwenyekiti

Certified true copy of the original.

25/6/1993

B. E. NYAMUBI,
Msajili

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 630

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI
(Katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam)

SHAURI LA MADAI NA. 32/1993

Maombi ya Barua ya Usimamizi wa Mirathi ya
Hassan Madiwa, Marehemu

na

Assia Hassan Hoza, Muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa wasia/Barua za Usimamizi wa mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu.

Mappingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 20 mwezi Oktoba, mwaka 1993.

Wasia wa marehemu huyo aliyetajwa umewekwa kwa amana na uwazi kwa upekuzi mahakamani.

Imewasilishwa Dar es Salaam tarehe 20 mwezi wa Julai, 1993.

Naibu Msajili

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 631

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI
(Katika Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mbeya.)

SHAURI LA MIRATHI NA. 2 LA MWAKA 1993

Maombi ya usimamizi wa Mirathi ya
Alimwene Mwasanjala wa Rujewa, Mbeya. Marehemu
na

Obasi Mwasanjala wa Rujewa, Mbeya, Mwombaji

TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kibali cha usimamizi wa mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu.

Mappingamizi yoyote kuhusu maombi hayo yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 3 Agosti 1993.

Imewasilishwa Mbeya leo tarehe 4 Juni, 1993.

A. A. SHAYO,
Msajili wa Wilaya Mbeya

Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka—(inaendelea kutoka ukurasa wa 369)

Wizara ya Viwanda na Biashara

Kuwa Maafisa Vipimo Daraja la II:—

- MAZIKU S. MWALWA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
- G. C. M. MWADUMLA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
- WILSON W. KACHOLI, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
- L. G. KULINDWA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
- E. E. ASENKA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
- STEPHEN VALERIAN, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
- M. B. M. SANGA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
- JOHN M. P. TINDIKA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
- F. M. F. NKUBA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
- R. E. KADEGE, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
- T. F. MBOMA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.

K. A. NYANDU, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 V. B. NDUKA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 K. Y. MWINJUMA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 D. E. MANZI, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 B. A. N. MICHAEL, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 J. K. SWAI, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 J. S. DOTTO, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 J. J. MUSHI, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 E. K. NYANDA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 A. A. NZAGA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 A. A. MAZIKU, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 STELLA R. H. KAHWA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 ADAM S. SALUO, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 SEBASTIAN GABRIEL, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 AMANI EMMANUEL, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 DAVID J. MAKUNGU, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 R. N. MBONABUCHA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 PETER R. CHUWA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 A. Y. MBWAMBO, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 H. C. KIPENGULE, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 ALEX C. K. SENEDA, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.
 EVARIST D. G. MASENGO, Afisa Vipimo Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1993.

Kuwa Mafisa Vipimo Daraja la I:—

S. S. F. KIBIKI, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 M. MWINYIMVUA (BIBI), Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 W. MBISE, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 F. N. MBALILO, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 S. B. MUTASHOBYA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 P. A. J. MASSAWE, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 A. M. MWAKILOVELE, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 J. A. MAYEGAS, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 C. E. S. SAWE, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.

P. S. MASINGA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 H. K. HAMIDU, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 N. K. T. MWANAGINDU, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 M. A. MBINGA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 R. M. ZEPHANIA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 M. P. URASA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 F. F. B. MATATA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 G. R. OLDEAN, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 C. H. KAAYA (BI.), Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 N. D. NG'ENI, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 B. G. M. KARUTA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 S. M. SAROTA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 FESTO P. PAUL, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 M. W. K. ABRAHAM, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 E. H. SILAS, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 P. NKWABI, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 R. K. A. MUTEGOA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.

D. M. NKYA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 E. A. MACHA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 G. NICHOLAS, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 J. D. MSENGEZI, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 H. HUSSEIN, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 L. P. S. SHIRIMA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 P. F. S. MASANJA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 W. M. KIMARO, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 B. S. URAGHUTU, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 H. E. MNENEY, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 OPTAT S. LYIMO, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 N. H. S. KAPOLI, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.
 M. CHUWA, Afisa Vipimo Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Juni, 1993.

MASAHIHISHO

Taarifa ya Kawaida Na. 170 Gazeti la Serikali Na. 10 la tarehe 5 Machi, 1993. Ongeza jina la Mtahiniwa No. TASI/1—206—IDI OMARI, T/A I, Box 9201 DSM, na sasa atangazwe kwamba amefaulu mtihani wote kwa kurudia somo alilokuwa ameshindwa hapo nyuma.

MASAHIHISHO—(inaendelea)

Taarifa ya Kawaida Na. 171 Gazeti la Serikali Na. 10 la tarehe 5 Machi, 1993.

Ondoa jina la mtahiniwa Na KC/3—217, ERNEST R. KALUNGWANA na badala yake weka jina la SALIMINI S. B. KHALFANI wa S.L.P. 178, Tanga.

Taarifa ya Kawaida Na. 172 Gazeti la Serikali Na. 10 la tarehe 5 Machi, 1993.

Mtahiniwa Na. KK/1—2197, BAKARI HAMISI wa S.L.P. 9124, D'Salaam. Katika taarifa ya Kawaida Na. 172 ya Gazeti lililotajwa hapo juu sasa atangazwe kwamba amefaulu mtihani wote kwa kurudia somo aliloshindwa hapo nyuma.

Taarifa ya Kawaida Na. 172 Gazeti la Serikali Na. 10 la tarehe 5 Machi, 1993.

Mtahiniwa Na. KK/2—2042, ELIZABETH M. JEMENI wa PHN S.L.P. 42, Mbinga. Katika taarifa ya Kawaida Na. 172 ya Gazeti lililotajwa hapo juu sasa atangazwe kwamba amefaulu mtihani wote kwa kurudia somo aliloshindwa hapo nyuma.

Taarifa ya Kawaida Na. 172 Gazeti la Serikali Na. 10 la tarehe 5 Machi, 1993.

Mtahiniwa Na. KK/1—2088, PETER B. MHINA (ASP) wa S.L.P. 9141, Dar es Salaam. Katika taarifa ya Kawaida Na. 172 ya Gazeti lililotajwa hapo juu sasa atangazwe kwamba amefaulu mtihani wote kwa kurudia somo aliloshindwa hapo nyuma.

Taarifa ya Kawaida Na. 192 Gazeti la Serikali Na. 10 la tarehe 6 Machi, 1992. Mtahiniwa Na. KK/1—1234, JEREMIA CHIZUWA, S.L.P. 1776 Dodoma.

Katika taarifa Na. 192 ya Gazeti lililotajwa napo juu, sasa atangazwe kwamba amefaulu mtihani wote kwa kurudia somo alilokuwa ameshindwa hapo nyuma.